Theofania ni neno la kiyunani lenye muunganiko wa maneno ya mawili “theos (Mungu)” na “faino (kuonekana)”. Hivyo ukiunganisha linazalika neno “kuonekana kwa Mungu”

Theofania sio kuonekana kwa Mungu katika ule utimilifu wake wote, hapana, kwasababu maandiko yanasema hakuna mtu awezayo kumwona Mungu akaishi (Kutoka 33:20). Hivyo Theofania ni njia mbadala (isiyo ya moja kwa moja) ambayo Mungu  aliitumia kujitokeza na kuongea na watu, kuthibitisha agano lake, au kuwapa maagizo.

Mfano wa njia hizo,

> Ni kijiti cha moto, alichotumia kuzungumza na Musa kule jangwani. (Kutoka 3)

> Mtu Yule aliyeshindana na Yakobo mweleka (Mwanzo 32:24-30)

> Melkizedeki (Mwanzo 14: 18-20)

> Yule mtu wanne aliyewatokea Shedraka, Meshaki na Abednego ndani ya moto (Danieli 3)

> Nguzo ya moto na wingu jangwani (Kutoka 13:21-22)

> Mungu kumtokea Samweli  (1Samweli 3:10)

> Maono ya Ezekieli (Ezekieli 1)

Je! theofania ipo hadi sasa?

Yesu Kristo alipozaliwa katika mwili, sio tena theofania, Bali ni utimilifu wote wa Mungu katika mwili.

> *Wakolosai 2:9 Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.*

Hapo mwanzo watu hawakumwona Mungu katika utimilifu huo, kwasababu kama wangemwona Mungu wangekufa kwasababu ya dhambi. Lakini Kristo alipokuja kuondoa dhambi kwa damu yake, wanadamu wote tunamwona Mungu katika utilimilifu wote, kwa Roho Mtakatifu aliyemweka ndani yetu.

Tunakikaribia kiti cha rehema, na neema kwa ujasiri bila kufa

kama kule mwanzo, kwasababu damu ya Yesu inanguvu ya kuzificha dhambi zetu zote. Ukimwona Kristo(moyoni) umemwona Mungu (Yohana 14:6-11)

Ndio maana ni kwanini leo hii mtu huwezi kumfikia Mungu bila Yesu Kristo.

Okoka leo upokee neema hii, ikiwa upo tayari kufanya hivyo, basi fungua hapa kwa mwongozo wa sala ya toba. >>>> KUONGOZWA SALA YA TOBA

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

> *Theolojia ni nini?. Na je ni sahihi kuisoma?*

> *Mwanazuoni ni mtu gani kibiblia?*

> *NINI TUNAJIFUNZA KWA THEOFILO MTUKUFU?*

Share on:
WhatsApp